SEHEMU YA SITA

JINSI YA KUWAFIKIA KWA NIABA YA YESU.

LENGO : KUJIFUNZA NJIA RAHISI YA KUENEZA INJILI NA KUANZA KUITUMIA MARA MOJA.

1. MWACHE MUNGU AUJAZE MOYO WAKO KWA WALE UNAOTAKA KUWALETA KWA YESU.

A. Uwapende kutosha kuyalilia maisha yao ya baada ya kifo, iwapo hawamkubali Yesu.
B. Ujali kutosha kuwaombea kwa imani ili waokolewe.
C. UWETAYARI KUFUNGA KULA UNAPOOMBA na uyaombee mahitaji yao, na kuwasaidia, ukiweza.

II ISHI NA YESU MBELE YAO ILI WATAMANI IMANI NA FURAHA ULIZO NAZO.

A. Wanachokiona ndani yako kitawatia au kuwavunja moyo kuwa wakristo.
B. Unavyozidi kumdhihirisha Yesu maishani mwako ndivyo watakavyozidi kutaka hicho ulicho nacho.

III UTAMBUE KWAMBA HIVI NI VITA VYA KIROHO DHIDI YA SHETANI KWA ROHO HIZO.

A. Atajaribu kutumia kuahirisha, kupotoa mafikira, hofu na aibu, kukuzuia kushirikiana na wengine juu ya neno la Mungu.
B. Kumbuka kwamba si maneno yako au uwezo wako kujibu maswali yao utakaomshinda shetani, bali uwezo wa Mungu.
C. Hakikisha unashirikisha sala kwa Mungu ili avunje vuzuizi vyo vyote na uwezo wa shetani alio nao kwao.
D. Katika jina la Yesu, dai damu ya Yesu dhidi ya shetani.

IV WAPELEKE KATIKA IBADA ZO ZOTE, MIKUTANO AU MAFUNZO YA BIBLIA AMBAYO ITAWAPA FURSA YA KUMKUBALI YESU.

V. SHRIKIANA NAO UNAPOWASILIANA NAO.

A. Jumuika nao kwa huruma na uwasaidie kwa njia yoyote uwezayo ili kuwaondolea mizigo au shida - na hivyo kujipatia haki ya kushirikiana nao kuhusu Yesu.
B. Katika mazungumzo, waambie kuhusu cho chote Mungu amekufanyia maishani mwako, jinsi Mungu amekusaidia katika kifungu cha injili, na kadhalika.
C. Wasaidie washirikiane nawe kwa kuwaambia, kwa upendo, kwamba "Mungu amekuweka moyoni mwangu, na nimekuwa nikikuombea. Ni nini kimekuwa kikifanyika maishani mwako ndipo Mungu kakuweka moyoni mwangu?"

VI. MWOMBE MUNGU AKUPE UWEZO WA KUJUA WAKATI WA KUWAULIZA IWAPO WANGEPENDA KUMKUBALI YESU.

A. Mungu anapofungua mioyo yao, ongoza mazungumzo ya kuwaelekeza kumkubali Yesu.
B. Wakati mwingine watu huwa tayari kumkubali Yesu mara moja.
C. Walakini, huenda ikamchukua Mungu muda kuitayarisha mioyo mingine kupitia sala zako na kushirikiana kwako, kwa hivyo mwache akuongoze.
D. Mungu anajua wakati wa kuwauliza wafanye uamuzi utakaowafanya wamkubali, wala si kumkataa Yesu.

VII JINSI YA KUMWONGOZA MTU KWA YESU UKITUMIA BIBLIA.

A. Ikiwa kanisa lako, au shirika lako la kikristo lina mpango wa kueneza injili kwa wapotevu, litumie, ikiwezekana.
B. Ikiwa hakuna, hizi hapa ni injili zitakikanazo kwa uokovu wao.
C. Ikiwezekana waonyeshe injili zote katika Biblia ili wajue ni Mungu anayezungumza, si wewe.

INJILI KWA MTU UNAYEMWELEKEZA KWA YESU.

HITAJI LAKO

Mungu akutaka uwe wake; lakini umetenda dhambi kama watu wengine wote duniani, zinazokutenga na Mungu.

"Watu wote wametenda dhambi na wametindikiwa na utukufu wa Mungu." Waroma 3:23.

MGAWO WA MUNGU

Lakini Mungu alikupenda sana kwamba alimtoa mwanawe Yesu kulipia dhambi zako kwa damu yake msalabani.

"Lakini Mungu amethibitisha kwamba anatupenda, maana tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu." Waroma 5:8.

Hisani ya Mungu, ambayo hatukuistahili, ilikupatia njia ya uokovu.

"Maana kwa damu yake Kristo, sisi tumekombolewa, yaani dhambi zetu zinaondolewa. Ndivyo ukuu wa neema yake." Waefeso 1:7.

Yesu alisema katika Yohana 14:6 kwamba yeye ndiye njia ya pekee ya kwenda kwa Mungu.

"Hakuna awezaye kwenda kwa Baba ila kwa kupitia kwangu."

"Binadamu hawakupewa jina la mtu mwingine ambaye tunaweza kuokolewa. Matendo 4:12.

WAJIBU WAKO

Yesu alikuwa duniani akihubiri toba na imani, ambavyo ni vitu viwili lazima ufanye ili uokolewe kutoka dhambi zako.

"Wakati umewadia, na ufalme wa Mungu umekaribia. Tubuni na kuiamini habari njema." Mariko 1:15

Baada ya Yesu kulipia dhambi zako kwa kusulubiwa, Mungu alimfufua kutoka wafu: kwa hivyo kumwamini ni kumkiri Yesu aliyekufuka, utaokoka.

"Ukiri kwa kinywa chako kwamba Yesu ni Bwana, na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka wafu, utaokoka. Warumi 10:9.

Kumbuka, hakuna cho chote waweza kufanya kitakachokuokoa.

"Maana, kwa neema ya Mungu mmekombolewa kwa njia ya imani.
Jambo hili si matokeo ya juhudi zenu, bali ni zawadi ya Mungu.
Wala halitokani na matendo yenu wenyewe, asije mtu akajivunia kitu. Waefeso 2:8-9

MAISHA YAKO YA MILELE

Yesu alituahidi kwamba tukimwamini tutakuwa na uzima wa milele naye mbinguni.

"Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili anayemwamini asipotee bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16.

Waweza kujua kwa uhakika kwamba utakwenda kuwa naye mbinguni utakapokufa.

"Nawaandikia mpate kujua kwamba mnao uzima wa milele ninyi mnaoniamini kwa jina la mwana wa Mungu." 1 Yohana 5:13

OMBENI SALA HII NAO KWA SAUTI KUBWA

1. Baba mpendwa uliye mbinguni, nakiri kwamba mimi ni mwenye dhambi.
2. Tafadhali nisamehe dhambi zangu zote.
3. Naamini kwamba Yesu alinilipia dhambi zangu zote kwa damu yake msalabani.
4. Namkubali Yesu kuwa mwokozi wangu na Bwana wa maisha yangu.
5. Naamini kwamba Yesu anaishi ndani yangu, nimesamehewa na sasa mimi ni mkristo.
6. Najua kwamba nitakwenda kuwa na Yesu nitakapokufa.

VIII SASA TUFANYE NINI?

A. Mwambie muumini mpya ampate mara moja mtu wa kumwambia yale Yesu amemfanyia maishani mwake.
B. Pangeni pamoja mkutano wenu ufuatao.
C. Ahidi kuendelea kumwombea, na atimize ahadi hiyo.
D. Mwaambie jinsi ya kuwasiliana nawe wanapotaka kufanya hivyo.
E. Waonyeshe jinsi ya kukua katika Kristo kwa:
   1. Kusoma Biblia kila siku.
   2. Kuzungumza na Mungu kwa sala wakati maalum kila siku.
F. Waanzishie vizuri mafunzo ya Biblia.
G. Waalike kanisani mwako, au wasaidie kushiriki mara moja katika kanisa watakalo.
H. Ikiwa hakuna kanisa, shirikianeni na wakristo walioko karibu kuunda kundi, kujifunza Biblia, kusali na kumwabudu Mungu.
I. Wasaidie kuunda vikundi vya watu watatu ili nao waanze mara moja kuwaombea rafiki na wapendwa wao waliopotea.
J. **Katika kikundi chako, mshangilie na kumsifu Mungu kwa mkristo huyu mpya, na uorodheshe jina la mtu mwingine asiyemjua Yesu kuchukua mahala pa huyo mkristo mpya.**

USHIRIKA WA KIMATAIFA WA WANAWAKE WA MWAKA 2000.

Ushirika wa wanawake wa kimataifa wa mwaka 2000 ni sehemu ya ushirika wa mwaka wa 2000 baada ya Kristo na baadaye, ambao unaendelea kuenea kwa haraka kote ulimwenguni. Lengo lake ni kuwafikishia neno la Yesu wale ambao hawajalisikia kufikia mwaka 2000 kwa kutoa 'kanisa kwa kila watu na injili kwa kila mtu.' Ushirika huu unawalenga zaidi ya watu billioni mbili wanaoishi na kufa bila kamwe kuisikia risala ya uokovu ya Yesu Kristo, na pia wale walioko karibu nasi ambao bado wamhitaji Yesu. Elfu kadha za mipango ya kueneza injili kufikia mwaka 2000 imefanywa katika madhehebu na mashirika ya kikanisa katika miaka ya hivi karibuni.

Wengi huamini kwamba kufikia mwaka 2000 tutaweza kulifikia eneo la mwisho la dunia ambalo halijafikiwa na risala ya mapenzi ya Kristo. Roho wa Mungu anawaunganisha wakristo kote ulimwenguni kufanya kazi ya kutekeleza njozi.

Ushirika wa wanawake wa kimataifa wa mwaka 2000 ni mmojawapo wa mashirika 16 duniani na huwaunganisha wanawake bila kujali madhehebu, taifa na miiko ya kikabila. Umegawanywa katika mabara yote kote duniani. Mashirika haya huwashirikisha viongozi muhimu wa wanawake, huhimiza na kufundisha sala kwa uenezi wa injili. Sala za vikundi vya watu watatu ni juhudi muhimu za shirika hizi.

Twaomba kwamba kitabu hiki kitakuwa mwanzo wa maombezi na uenezi wa injili, na kwamba maelfu na maelfu ya waombaji watasoma kanuni hizi na kuzitumia kuwaleta wapotevu kwa Yesu.

Judy Mbugua - *Mwenyekiti wa kimataifa*
Lorry Lutz - *Mshirikishi wa kimataifa.*

WASHIRIKI WA KIKUNDI CHA WATU WATATU CHA SALA

(Rarua na Ukunje)

KUNJA ▼

"Tena nawaambieni, wawili miongoni mwenu wakikubaliana hapa duniani kuhusu jambo lo lote la kuomba, Baba yangu wa mbinguni atawafanyia jambo hilo. Kwa maana po pote pale wanapokusanyika kwa jina langu, mimi nipo kati yao

Matayo 18:19-20

KUNJA ▼

VIKUNDI VYA WATU WATATU VYA SALA

KIKUNDI CHA WATU WATATU CHA MAOMBI NI NINI?

Ni njia rahisi na inayofaa ya kuwaleta watu wengine kwa Yesu. Unaungana tu na wakristo wawili na kusali pamoja mara kwa mara kwa uokovu wa rafiki tisa au jamaa wasiomjua Yesu, na nchi ambapo Yesu hajulikani. Kisha furahieni mnavyoona. Matayo 18:19-20

A Study Guide for Evangelism Praying by Evelyn Christenson © 1992 Kiswahili Chapter 6 scanned 14-Feb-04

A Study Guide for Evangelism Praying by Evelyn Christenson © 1992 Kiswahili Chapter 6 scanned 14-Feb-04

WASHIRIKI WA KIKUNDI CHA WATU WATATU CHA SALA

(Rarua na Ukunje)

KUNJA ▼ KUNJA ▼

MAELEKEZO

* Chagua wakristo wawili au jamaa kuunda kikundi cha sala.
* Kila mmoja wenu achague majina ya watu watatu wasiomjua Yesu kuwa mwokozi na Bwana wao. Chagua nchi ambapo Yesu hajulikani au ni haba.
* Kubaliana saa ya kukutana mara moja kwa juma kusali pamoja kwa watu wenu 9. Dakika 15 nyumbani kwako, kazini au shuleni, kabla au baada ya mkutano wa kadhalika zatosha.
* Ombeni pamoja kwa wale watu 9 kwa kuwataja majina yao kila mmoja ili waweze kumkubali Yesu mwokozi na Bwana wao, pamoja na mahitaji na upungufu wao binafsi. Pia iombee nchi yako.
* Inapowezekana, na kwa uongozi wa Mungu, shirikianeni kirafiki na wenzako watatu. Ombeaneni mnapojitayarisha kufanya hivyo.
* Rafiki zako wanapokuwa Wakristo, endeleeni kuwaombea, hata ikiwa kundi lako la watatu limeanza kuwaombea wengine.
* Ikiwezekana, washirikishe katika kanisa lako, mafunzo yenu ya Biblia na/au ushirika wenu baada ya wao

WASHIRIKA WANGU KATIKA SALA NI:

1. _____
2. _____

MAJINA MATATU YA KILA MMOJA WETU KUWAOMBEA

1. _____
2. _____
3. _____

1. _____
2. _____
3. _____

WATU AMBAO NAOMBA WASALIWE NI?:

1. _____
2. _____
3. _____

KUNDI LETU LA WATU AMBAO HAWAJAFIKIWA:

_____

❑ **Ndio, najitolea kuungana na watu wengine watatu kuunda kikundi cha sala cha watatu.**

Jina _____

Anwani _____

Mji _____

Ili tuweze kujua kuhusu juhudi zake maombini, tafadhali jaza fomu hii na uirudishe kwa:

Hakikisha umemwarifu mtu ambaye jina lake liko hapo juu wakati mtu anayeombewa na kikundi chako anamkubali Yesu.

Back cover

MWITO WA MUNGU KWA ULIMWENGU

Katika mwongo huu wa miaka ya tisini, mamia ya maelfu ya viongozi na watu wa kawaida kote ulimwenguni wameusikia mwito wa Mungu ukiwaita kwa lengo sawa na muda sawa.

Mwito wa Mungu ni kwa wakristo wayafikie makundi ya watu ambayo hayajafikiwa kote ulimwenguni, kwa injili ya Yesu. Muda unaotolewa kwa kazi katika mwito wa Mungu ni mwaka 2000.

Ijapokuwa jambo la mwisho Yesu alilowaambia wafuasi wake kabla ya kupaa mbinguni ni kwamba wawe mashahidi katika sehemu zote za ulimwenguni na sasa karibu miaka 2000 baadaye, agizo hilo halijatekelezwa.

Lakini kwa ghafla upo umuhimu unaoenea kote katika jamii ya wakristo, moja kwa moja kutoka kwake Mungu.

JE MUNGU AMEKUWA AKIUWEKELEA MWITO WAKE WA DHARURA MOYONI MWAKO?
IPO WASI WASI NDANI YA ROHO YAKO KWAMBA KUNA KITU ZAIDI?
AU UMEJARIBU KUWALETA WAPOTEVU KWA YESU, LAKINI HUKUFAULU?

Ikiwa ni hivyo, katika kitabu hiki, umo msaada huu kwako.

* Kufahamu sababu ya mwito wa Mungu kwako.
* Matayarisho yako binafsi yanayohitajika ili ufaulu kuutekeleza mwito wake.
* Maagizo kwa sala zako za nguvu kabla ya kuanza uenezi wa ijili.
* Jinsi ya kuombeana katika vita hivi vya kiroho.
* Maagizo rahisi kuhusu jinsi ya kuwafikia wale wasio na Yesu na wangali bado katika utawala wa shetani.
* Ambapo 90% ya wale ambao bado hawana ujumbe wa Yesu wanaishi katika eneo la dirisha la 10/40
* Jinsi ya kuwafikia wapotevu walioko karibu nawe nchini mwako, na pia katika sehemu za mipaka ya dunai.

Haya yote yamo katika kitabu hiki kilicho rahisi kufahamu.

MRADI WA SALA WA VIKUNDI VYA WATU WATATU.

"Kwa maana popote pale wanapokusanyika wawili au watatu kwa jina langu, mimi nipo hapo kati yao." Matayo 18:20

Translated by: Kweya Ayanga,
P. O. Box 11680 NAIROBI
Tel. 747413